



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



Mei 03, 2023

## TAARIFA KWA UMMA

MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA MHE. WISE MGINA  
AMETUMA SALAMU ZA SHUKRANI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSEN

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Mhe. Wise Mgina ametuma salamu za shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia fedha Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Milioni **977,600,000/=** chini ya Mradi wa Boost katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa imepokea fedha hizo tarehe 24 Aprili 2023 na fedha hizo zimegawanywa kama ifuatavyo; -

1. Kata ya Mavanga imepokea fedha ya kujenga Shule ya Msingi Mpya eneo la Ruhuhu Darajani kiasi cha jumla ya shilingi Milioni **347,500,000/=**. Aidha shule ya msingi Mbugani imepokea kiasi cha jumla ya shilingi **81,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na matundu 3 ya choo.
2. Kata ya Ludewa imepokea fedha ya kujenga madarasa 2 ya Elimu ya Awali katika shule ya msingi Ludewa Mjini kiasi cha jumla ya shilingi **69,100,000/=**
3. Kata ya Milo imepokea fedha ya kujenga madarasa 3 na matundu 3 ya choo katika shule ya Msingi Mapogoro kiasi cha jumla ya shilingi **81,000,000/=**
4. Kata ya Ludende imepokea fedha ya kujenga madarasa 3 na matundu 3 ya choo katika shule ya Msingi Maholong'wa kiasi cha jumla ya shilingi **81,000,000/=**
5. Kata ya Mlangali imepokea fedha ya kujenga madarasa 4 na matundu 3 ya choo katika shule ya Msingi Mlangali kiasi cha jumla ya shilingi **106,000,000/=**
6. Kata ya Mundindi imepokea fedha ya kujenga darasa 1 na matundu 3 ya choo katika shule ya Msingi ya Elimu Maalumu Mundindi kiasi cha jumla ya shilingi **31,000,000/=**
7. Shule ya Msingi Nindi iliyopo Kata ya Lupingu imepokea fedha kiasi cha jumla ya shilingi **181,000,000/=** kwaajili ya ujenzi wa madarasa 3, ujenzi wa matundu 3 ya choo na nyumba mbili za walimu.

Chrispin B. Kalinga  
**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini (W)  
LUDEWA.**

Ludewa ya Utalii, Uchumi wa Chuma na Makaa ya Mawe kwa Maendeleo Yetu.

---

Barua zote zitumwe kuititia anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, 3 Barabara ya Boman, S. L. P 19, **59401 NJOMBE**,  
Simu +255 26 2790120, Nukushi + 255 26 2790128, Baruapepe; [ded@ludewadc.go.tz](mailto:ded@ludewadc.go.tz), Tovuti [www.ludewadc.go.tz](http://www.ludewadc.go.tz)